**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
# CHUO KISHIRIKI CHA ELIMU DAR ES SALAAM
# SHULE YA SEKONDARI YA MAZOEZI CHANG'OMBE

NDUGU

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MCHEPUO WA --------------- MWAKA 2024/2025**

## 1.0 UTANGULIZI

Napenda kukutarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya kidato cha **TANO** katika shule ya sekondari Chang'ombe. ***Hongera Sana.***

## 1.1 KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 1/7/2024 fika na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Baada ya wiki mbili tokea tarehe ya shule kufunguliwa nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine.

## 1.2 MAHALI ILIPO SHULE

Shule ya Sekondari Chang'ombe ipo ndani ya eneo la Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (Zamani Chuo Cha Ualimu Dar es Salaam) katika Manispaa ya Temeke. Imepakana na Uwanja mpya wa Taifa.

## 2.0 USAJILI

Unatakiwa ufike shuleni tarehe 13/08/2023 asubuhi saa 2.00 ili upate kusajiliwa na kupatiwa maelekezo muhimu kuhusu shule, ukiwa pamoja na Mzazi/Mlezi.

**Mwanafunzi anatakiwa kuja na nakala ya Cheti cha Kuzaliwa na Matokeo ya Kidato cha Nne (Notification of Results).**

## 3.1 MICHANGO

- Mchango wa uendeshaji wa Shule — Tshs 35,000/=
- Vitambulisho — Tshs 5000/=
- Nembo — Tshs 5000 /=
- Tahadhari — Tsh 5000/=

**JUMLA 50,000/=**

Lipa michango hiyo hapo juu kwenye Akaunti Na. **071101000196** ya benki ya **NBC,** jina **ni "DUCE COLLECTION ACCOUNT" Kabla ya kufanya malipo utakwenda katika ofisi za Uhasibu kwa ajili ya kupata control namba.**

## 3.2 MAHITAJI MENGINE

- Karatasi Rimu moja $A_4$ ( Aina ya Monde au Rotatrim au Nopa au No.1)
- Kifaa cha Usafi : Wavulana – Ndoo Ya lita 10 na Wasichana - Fagio kubwa ndani(soft bloom)

## 3.3 VIFAA VINGINE KWA WOTE

- Kamusi (Dictionary)
- Nguo za michezo traki suti ya bluu bahari(wasichana)/Bukta na Tshirt yake zote za bluu bahari(wavulana tu),raba za michezo nyeupe/ kwa wanaocheza mpira wa miguu wanunue viatu vya mpira wa miguu.
- Begi la kubebea madaftari na vitabu
- Madaftari makubwa(counter book) matano (**5)** kwa wale wa PCB na Manne (**4)** kwa HGL na PCM.
- Koti la maabara (Kwa wanafunzi wa PCB na PCM)
- Dissection Guide (Kwa wanafunzi wa PCB)
- Vitabu mbalimbali kulingana na tahasusi husika

## 4.0 VAZI RASMI LA SHULE

a) **Wavulana :**suruali **Navy blue** mbili upana wa chini usipungue inchi 16, mashati meupe mawili mikono mifupi na tai mbili, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi, Mikanda miwili myeusi ya ngozi na soksi nyeusi.

b) **Wasichana :**sketi za **Navy blue** mbili mshono wa malinda box, mashati meupe mawili mikono mifupi na tai mbili, Viatu vyeusi vya ngozi na soksi nyeupe.

**Hijab kwa Waislamu:** Ushungi mweupe usio na mapambo na uvaliwe na shati jeupe

mikono mirefu (Nusu Kanzu) na sketi yake iwe ndefu.

c) T-shirt (Navy blue)

d) Tai (navy blue yenye mistari ya njano)

## 5.0 MENGINEYO MUHIMU

Matumizi na mahitaji ya mwanafunzi yanamtegemea zaidi Mzazi /Mlezi. Ni imani yetu kuwa utampa mwanao msaada wa kila aina ili aweze kusoma kwa makini na kwa ufanisi

***NB: Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya kwa utekelezaji fanisi. Shule haipo tayari kwa usumbufu wowote unaohusiana na mahitaji haya muhimu***

**MWISHO**
Uongozi wa Shule unakutakia maandalizi mema ya kujiunga na shule yetu.

Ni Matumaini yetu utazingatia kanuni na sheria za shule ili lengo lililokuleta shuleni liweze kukamilika.

*Kauli mbiu yetu ni* **"ELIMU NI MAENDELEO"**

**Karibu Sana.**

________________

ZAHARA SHABANI MUSTAPHA
MKUU WA SHULE

0789815318/0714889972

## SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na- 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na myingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

### *A: MAHUDHURIO:*

1. Kila mwanafunzi ni lazima afike shuleni asubuhi saa 12:30 na kufanya usafi wa mazingira na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili.
2. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka (Kutoroka) katika eneo la shule bila kupata kibali/ruhusa kutoka kwa mwalimu wa darasa au wa zamu. Aliyepata kibali ni sharti akionyeshe kwa mlinzi getini
3. Siyo ruhusa kwa mwanafunzi kukosa kufika shuleni bila kupata kibali.

Ruhusa itatolewa kwa sababu maalum tu na hata hivyo mzazi/mlezi

Analazimika kufika kuomba ruhusa na kujieleza kimaandishi. Mwanafunzi akikosa zaidi ya siku tatu mfululizo atalazimika kufika mbele ya kikao pamoja na mzazi/mlezi ajieleze. Ieleweke kwamba ni mwanafunzi na siyo walezi wa bandia

4. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo na usalishaji mali atakavyotakiwa na ratiba bila kuchelewa
5. Mwanafunzi ni lazima afanye mitihani ya masomo yote aliyosoma

***B: TABIA NA MWENENDO***

1. Kila mwanafunzi lazima awe na nidhamu ya hali ya juu kuwaheshimu wafanyakazi wote na wanajumuiya kwa jumla. Mwanafunzi asiye na nidhamu atapoteza nafasi yake.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:

   i. Kuvaa Pete
   ii. Kunyoa nyusi
   iii. Kuvaa Hereni
   iv. Kupaka Hina na Rangi za Kucha
   v. Kuwa na Kucha ndefu
   vi. Kuweka dawa nywele.
   vii. Kunyoa kipara au mitindo
   viii. Kuwa na simu za mkononi shuleni.
   ix. Kuvaa mlegezo wa Sketi au Suruali
   x. Kuwa na ndevu
   xi. Kuvaa rozari au tasbihi

3. Makosa yafuatayo yatapelekea mwanafunzi kuadhibiwa na kuonywa;
   i. Uchelewaji wa sehemu yoyote anapohitajika
   ii. Kutofanya kazi za usafi wa mazingira
   iii. Kutojali masomo na uzalishaji mali
   iv. Mwanafunzi anazo nafasi mbili tu za kuonywa na baada ya hapo kikao kinachohusika kitamchukulia hatua kali zaidi.

***C:*** Makosa yanayoweza kumfukuzisha/kumsimamisha mwanafunzi bila ya kuonywa

- Wizi
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
- Ubakaji, Uasherati na ushoga
- Ulevi
- Kuoa au kuolewa
- Utoro
- Kupata au kutoa mimba/ Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- Ushirikina
- Kuua
- Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- Dharau,ukaidi,ubishi,utoro,uvivu,upigaji kelele,kukaa maeneo

yasiyoruhusiwa

- Kuharibu mali ya shule
- Kupigana, kupiga
- Kutukana
- Kuvuta bangi na madawa ya kulevya, uvutaji sigara, kamari.
- Makosa ya jinai
- Kukashifu viongozi na kudharau bendera ya Taifa.
- Kukataa adhabu kwa makusudi.

***D: MALI ZA SHULE***

1. Mwanafunzi akikabidhiwa vifaa kama vitabu vya kusomea. Anatakiwa kuviangalia sana na sharti virudishwe kwa mwalimu aliyekambidhi kila vinapohitajika kurudishwa.
2. Ieleweke kwamba ni kosa kubwa sana kuharibu mali yeyote ya shule ikiwa ni pamoja na majengo. Adhabu yake ni gharama ya kulipishwa (faini) na kufukuzwa.
3. Kifaa chochote kitakachopotea sharti kilipwe. Cheti cha kumaliza shule Hakitatolewa kwa yeyote ambaye hatarudisha au kulipa vifaa alivyokabidhiwa.
4. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na begi la kubebea na kuhifadhi madaftari/vitabu. Hairuhusiwi kubeba madaftari/vitabu mkononi au mfuko wa aina nyingine yoyote.

**KIAMBATISHO**

**SHULE YA SEKONDARI YA MAZOEZI CHANG'OMBE**

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI**

| |
|---|
| **PICHA YA MWANAFUNZI** |

**A. IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. **Jina kamili la mwanafunzi ……………………………………………………………..**
2. **Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………………………**
3. **Mahali Alipozaliwa …………………………(Wilaya) ………………………………(Mkoa)**
4. **Taifa ……………………………………………………………………………………….**
5. **Uraia ………………………………………………………………………………………**
6. **Dini ……………………………………………………………………………………….**
7. **Shule alizosoma/aliyosoma kabla ya kuja shule ya Sekondari Chang'ombe**

| **Jina la Shule ya Msingi/ Sekondari** | **Tarehe aliyoanza** | **Tarehe aliyomaliza** |
|---|---|---|
| **i** | | |
| **ii** | | |
| **iii** | | |

| iv | | |
|---|---|---|

Sahihi ya mwanafunzi ………………… Tarehe ……………

## B: MAELEKEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

**PICHA MZAZI/MLEZI**

1. **Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………………………………………**
2. **Utaifa ……………………………………………………………………**
3. **Uraia …………………………………………………………………….**
4. **Anuani ya DSM …………………………………… ……….**
   **…………………………………………………………………………….**
5. **Sehemu anayoishi ………………………………………………………**
6. **Mtaa ……………………………………………………………………**
7. **Namba ya nyumba ……………………………………………………...**
8. **Simu: Nyumbani…………………………………………………**
   **Ofisini ………………………………………………………**

   **Mkononi …………………(Ikibadilika toa taarifa)**

**Eleza kama mtoto ana matatizo yoyote ya kiafya ……………………………………..**

**……………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

## C: MAELEZO YA KIKAZI (Mzazi/Mlezi)

i. **Jina la Mwajiri ……………………………………………………………………..**
ii. **Anuwani ……………………………………………………………………………..**
iii. **Kazi ya mzazi/Mlezi ……………………………………………………………**
iv. **(Mfano,Karani,Mwalimu n.k)**

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……………………………… Tarehe…………………….**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**CHANG'OMBE DEMONSTRATION SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be filled by Government Medical Officer and return to the **HEAD OF SCHOOL CHANG'OMBE SECONDARY SCHOOL**, P. O. BOX. 2329, DAR ES SALAAM

To the Medical Officer

…………………………….

……………………………..

……………………………...

A: RE:
…………………………………………………………………………………………………

**Please examine the above mentioned student. Comment on his/her fitness by responding to the problems below.** Say **Yes** or **No** to each problem and if yes then state**:**

………………….
Head of School

Date………………….

Please insert (**v**) in the boxes provided

| | | |
|---|---|---|
| i Hearing | yes [ ] | No [ ] |
| ii Speech | yes [ ] | No [ ] |
| iii Sight | yes [ ] | No [ ] |
| iv T.B. | yes [ ] | No [ ] |
| v B.P | yes [ ] | No [ ] |
| vi Diabetes | yes [ ] | No [ ] |
| vii Mental case | yes [ ] | No [ ] |
| viii Physical disability | yes [ ] | No [ ] |

Ix Any other
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

B: Recommend if the student is fit for studentship (i) Yes (ii) No

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
……

C: Any other advice

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………....

………………………………………………

Name, Designation and Signature Date …………………
Stamp……………………..

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI**

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANG'OMBE,

S.L.P 2329,

**DAR ES SALAAM.**

**TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi (Mwanafunzi) ………………………………………………………………………(Jina kamili)

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha …………….............. Mchepuo ……………………..

Mwaka…………………………. katika Shule ya Sekondari Chang'ombe.

**Ninaahidi kwamba:**

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za kishule.
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyo bora bila kushurutishwa.
4. Sitaitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza malighafi (raw materials)
5. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Sekondari Chang'ombe.

**Saini ya Mwanafunzi** …………………..……………. **Tarehe** …………………………

## TAMKO LA MZAZI/MLEZI

Mimi ( Jina kamili la Mzazi/Mlezi) ………………………………………………………………..

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………………….

**Naahidi kwamba**

1. Nitampatia mtoto wangu mahitaji yote muhimu ya shule kama yalivyoelezwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
2. Nitakua tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni,adhabu n.k)katika kumlea mtoto wangu
3. Nitamhimiza mtoto wangu kusoma kwa bidii, kufanya mazoezi ya masomo yake (Home work) na **kufuatilia maendeleo na tabia yake shuleni**.
4. Mtoto wangu akiwa nyumbani nitamlea katika maadili mema anayostahili ili awe mfano mzuri shule na katika jamii kwa ujumla.

**Saini ya Mlezi/Mzazi** …………………..………… **Tarehe** ………………………